(Na Mpigapicha Wetu).



# Wavuvi wafurahia soko jipya la samaki

**Na Peti Siyame, Kalambo**

WAVUVI wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa wamefurahia kujengewa soko la kisasa la samaki lililopo mwambao mwa Ziwa Tanganyika katika Kata ya Kasanga wilayani Kalambo.

"Kwa zaidi ya miaka minane, sisi wavuvi tulikuwa tukitumikishwa na wamiliki wa kampuni za uvuvi zilizopo katika Mji wa Mpulungu mwambao mwa Ziwa Tanganyika upande wa Zambia.

"Walikuwa wakitupatia maboti ya uvuvi, injini, mafuta na zana bora za uvuvi, sasa kuvua lazima tukawauzie lakini kwa bei wanayopanga wenyewe," alisema mmoja wa wavuvi hao, Joseph Sichilima.

Kauli yake hiyo iliungwa mkono na wavuvi wengine wakiwemo John Sikazwe na John Chifunda.

Soko hilo ambalo ujenzi wake uligharimu Sh 802,488,528 lilifunguliwa rasmi Februari 23, mwaka 2012 na aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais, Dk Mohamed Gharib Bilal.

Ujenzi wake ulianza Desemba mwaka 2009 na kukamilika mwaka 2011 ambapo kiasi kikubwa umefadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU).

Lilijengwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (Mviwata) kwa kushirikiana na GRET na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kabla ya kugawanywa na kuundwa Halmashauri ya Kalambo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Wilaya ya Kalambo, Palela Msongela akizungumza na wavuvi hao sokoni hapo, aliwapatia miezi miwili kufanya shughuli zao bila kulipia ushuru.

Alisema utaratibu uliopo wavuvi wakivua samaki wabichi watakuwa wakihifadhiwa katika chumba cha barafu kabla ya kuwauza kwa wajasiriamali wanawake ambao watawauzia wateja.

Akifafanua alisema kutakuwa na minada mitatu itakayofanyika sokoni hapo kila Jumapili, Jumanne na Alhamisi.

"Changamoto kubwa ni kwamba soko halina chumba kinachohifadhi baridi kali chenye uwezo wa kuhifadhi samaki kwa dakika chini ya 30," alisisitiza.

Aliitaja changamoto nyingine kuwa soko linafurika maji pindi maji ziwani yakijaa ambapo miundombinu iliyopo haiwezi kupitisha maji hayo ya kuyamwaga umbali mrefu kutoka hapo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Soko, Kennedy Sinyangwe alisema takribani watu 70,000 wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka eneo hilo wanashughulika na uvuvi.

Aliongeza wastani wa tani 170,000 za samaki zinavuliwa kwa mwaka na changamoto kubwa iliyokuwepo ilikuwa kutokuwepo kwa soko la uhakika lenye ushindani.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akizungumza wakati wa ufunguzi wa kongamano la vijana kuhusu kilimo mjini Chato mkoani Geita juzi ambalo lilishirikisha vijana kutoka mikoa ya Shinyanga, Kagera na Geita. (Na Mpigapicha Wetu).

jwa huo utakapodhibitiwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Balozi Wilbert Ibuge alisema ajenda ambazo

China, wapo salama.

Mpaka sasa nchi 101 kati ya 194 duniani zimeathirika kwa ugonjwa huo. China na Italia zinaongoza kwa maambukizi na vifo vingi.

# Ukaguzi wanaokata nyama kwa magogo leo

Na Lucy Lyatuu


BODI ya Nyama Tanzania (TMB) imesema kuwa kuanzia leo itaanza ukaguzi wa bucha zinazoendelea kutumia magogo kukata nyama.

Kaimu Msajili wa TMB, Iman Sichalwe alisema jana alipozungumza na HabariLEO kuwa vikao vya kujipanga kwa utekelezaji huo vinaendelea.

Aliitaja mikoa itakayoanza ukaguzi wa bucha zinazotumia magogo ni Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Manyara, Mbeya, Singida na Morogoro.

"Tumepanga watu wa ukaguzi, muda wowote wataanza kwani hata barua kutoka Tamisemi zimesambazwa," alisema Sichalwe akiongeza wamejipanga na wataalamu wao na wa Jiji.

Alisema magogo katika kukata nyama sio mazuri kiafya ndio maana bodi imekuwa ikipinga kuendelea kutumika katika mabucha.



Aliwataka wauzaji wa nyama kujitayarisha na utekelezaji wa kanuni mpya zinazowataka kuachana na utumiaji magogo kukata nyama.

Bodi ya Nyama imesema matumizi ya magogo yanatishia afya za walaji na kutaka wamiliki kutafuta mashine za umeme za misumeno.

"Yale magogo ya kukatia nyama huhifadhi uchafu wa mabaki ya nyama na vijidudu na baadaye huleta magonjwa kwa walaji," alisema.

Kuanzia Septemba mwaka jana bodi hiyo ilisema mwisho wa kutumia magogo ya kukatia nyama ni Septemba 30, mwaka jana.

Ilielezwa magogo hayo husababisha upotevu wa nyama, katika kilo 100 kilo moja hupotea na kwa mwaka muuzaji anapoteza Sh milioni 3.8 inayotosha kununua mashine ya kisasa kukatia.

Scanned by CamScanner

UFUGAJI

# Watakiwa kufuga kuku, nguruwe

**Dar es Salaam.** Wafugaji nchini wametakiwa kuwekeza zaidi katika kuku na nguruwe ili kuziba pengo la upungufu wa nyama nyekundu kwa tani 130 unaotarajiwa kutokea mwaka 2022.

Wito huo umetolewa na Katibu Mkuu Wizara Mifugo, Elisante Ole Gabriel katika mkutano wake na vyama vya wafugaji kuku, nguruwe na wadau wa ngozi.

Alisema wadau wanapaswa kuchukulia changamoto hiyo kama fursa ya kujiingizia kipato zaidi.

"Mara zote huwa tunasema changamoto inapotokea sehemu moja ni fursa kwa upande wa pili, nadhani ni wakati muafaka wadau wawekeze katika sekta hii ya nyama nyeupe," alisema Ole Gabriel.


"Kufanya hivi kutatuhakikishia kuwa tunafidia hayo mahitaji yanayohitajika. Lakini bado ulaji wa nyama kwa Watanzania uko chini, nitumie fursa hii kuhamasisha watu waongeze kiwango (cha kula nyama)."

Alisema kwa mujibu Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) mtu mmoja anatakiwa kula kilo 50 za nyama kwa mwaka huku wakati kwa Tanzania mtu mmoja anasadikika kula wastani wa kilo 15 kwa mwaka.

"Sasa niwaombe Watanzania, ili hawa watu wanaotaka kuwekeza katika nyama nyeupe waweze kufanikiwa ni vyema tujifunze kula vya kwetu, kwa nini tunaanza kutafuta kuku kutoka nje wakati tuna kuku milioni 79, kwa nini tuagize mayai kutoka nje.

"Tujifunze kupenda vyetu na nyama nyeupe ina faida kwa sababu kiafya inaaminika kuwa haina lehemu ndiyo maana watu wengi wanahamia katika matumizi ya nyama hiyo," alisema Ole Gabriel Gabriel.

***(Aurea Simtowe)***





Pngowi2002@yahoo.com.
0 754 653 740



Aurea Simtowe

Scanned by CamScanner

# Wafugaji washauriwa kuzingatia ubora mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewataka wafugaji nchini kuzingatia ubora wa mifugo na sio wingi ili kupata mazao yenye kuwanufaisha kiuchumi.

Prof. Ole Gabriel, alitoa wito huo jijini Dodoma jana, wakati akiwakaribisha wawekezaji wa kampuni ya kuchakata na kusambaza nyama ya Tanfroz Limited inayomilikiwa na wawekezaji kutoka Ubelgiji na Ufaransa, walipofika ofisini kwake kujitambulisha.

Alisema kubadilika njia ya ufugaji kutoka wa uchungaji kwenda wa kisasa unaozingatia sayansi utamletea tija mfugaji na kunufaika kiuchumi.

Prof. Gabriel alisema azma ya serikali inasisitiza uchumi wa viwanda na haiwezi kufanikiwa bila kuboresha sekta ya mifugo, ambayo hutegemewa kwa malighafi za viwandani.

Katibu Mkuu huyo aliwaahidi kutoa ushirikiano na wataalamu wake katika hatua mbalimbali za kuanzisha mradi wa ufugaji, ambao utawanufaisha Watanzania.

Mradi huo umeanza kwa majaribio mkoani Iringa katika eneo la Mgagao ambako kuna shamba lenye ng'ombe zaidi ya 200.

Mkurugenzi wa kampuni ya Tanftoz Limited, Luc Battel, alisema Tanzania ina fursa kubwa ya uwekezaji katika sekta ya mifugo kutokana na wingi wake.

Alisisitiza kupata mifugo yenye ubora ni lazima kuwapo na utaratibu unaokubalika kitaifa na kimataifa.

Alisema kupitia mradi huo, Tanzania itafanikiwa kupata masoko ya nyama katika nchi za mashariki ya mbali na sehemu mbalimbali duniani.

Aidha, alisema uboreshaji wa mazao yatokanayo na mifugo kama nyama, maziwa na ngozi ni jambo muhimu kutumika kama malighafi.

Meneja wa kampuni ya CRV, Hielke Sportel, alisema kuwa ni vema wafugaji wakawa na ushirikiano katika kubadilishana habari na elimu mbalimbali za ufugaji bora wenye tija.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti nchini (TALIRI), Dk. Eligy Shirima, aliwashukuru wawekezaji hao kwa kutambua fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya mifugo na kuahidi kuwapa ushirikiano kila inapohitajika ili kuwainua wafugaji nchini.

Scanned by CamScanner

waathirika

WAJENGEWE UELEWA

Jeremiah Wandili, Katibu Mkuu wa Mtandao wa Asasi za Kiraia Kinondoni, alisema msingi wa kukabiliana na athari hizo ni kujenga uelewa kwa wananchi kwani wao ndio waathirika wakubwa.



**WANAOTUHUMIWA kuishi nchini kinyume cha sheria , wakipanda lori la Idara ya Uhamiaji, baada ya kukamatwa katika maeneo mbalimbali, Dar es Salaam, juzi.**(Picha na Christopher Lissa).

# Wafugaji watakiwa kuzingatia ubora wa mifugo, sio wingi

**Na MWANDISHI WETU**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel, amewataka wafugaji nchini kuzingatia ubora wa mifugo kwani ndio utawanufaisha kiuchumi, sio wingi wa mifugo.

Akizungumza jana, Jijini Dodoma, wakati akiwakaribisha wawekezaji wa kampuni ya kuchakata na kusambaza nyama ya Tanfroz Limited, inayomilikiwa na wawekezaji kutoka nchini Ubelgiji na Ufaransa, Profesa Elisante, alisema mfugaji atakapoanza ufugaji wa kisayansi na kuanza kupata mazao ya mifugo yaliyo bora, ndipo atakapoanza kufaidika na kazi ya ufugaji.

"Azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, inayosisitiza uchumi wa viwanda, haiwezi kufanikiwa vizuri bila kuboresha mifugo, ambayo mazao yake hutegemewa kama malighafi za viwandani,"alisema.

Profesa Elisante aliwaahidi wawekezaji hao ushirikiano katika hatua mbalimbali kwa lengo la kufanikisha mradi huo, ambao ukishaanza rasmi, utawanufaisha wawekezaji na wafugaji wa hapa nchini na kwa majaribio, alisema mradi huo umeanzia mkoani Iringa katika maeneo ya Mgagao, ambako kuna shamba lenye ng'ombe zaidi ya 200.

> **"Azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, inayosisitiza...**
>
> Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel

Akizungumza kwa niaba ya kampuni hiyo, Mkurugenzi wa Tanftoz Limited, Luc Battel, alisema Tanzania ina fursa kubwa ya uwekezaji katika sekta ya mifugo kutokana na wingi wa mifugo iliyopo nchini.

Alisistiza kuwa mifugo yenye manufaa ni ile yenye ubora unaotakiwa kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi huyo alisema Tanzania itafanikiwa kupata zaidi masoko ya nyama katika nchi za mashariki ya mbali na kwingineko duniani iwapo tu ng'ombe au mbuzi watafugwa katika mazingira bora na kuepushwa na maradhi, yakiwemo magonjwa ya miguu na midomo.

Aliongeza kuwa uboreshaji wa mbari ni muhimu katika kupata mazao bora ya mifugo kwa maana ya nyama, maziwa na ngozi, ambayo hutumika kama malighafi katika viwanda mbalimbali hapa nchini.

"Ili kufanikiwa katika uboreshaji wa mbari nchini, ni vema wafugaji wakawa na ushirikiano katika kubadilishana mbari na elimu mbalimbali za ufugaji bora wenye tija," alisema.

Scanned by CamScanner